بسم الله الرحمن الرحيم

## Jibu la Swali

## Ni Yapi Yaliyo Nyuma ya Ongezeko la Mgogoro wa Yemen
**(Imetafsiriwa)**

**Swali:**

Baada ya vikosi vya Baraza la Mpito la Kusini (STC) nchini Yemen, vikiongozwa na Aidarus al-Zubaidi, mjumbe wa Baraza la Rais, kupeleka vikosi vyao huko Hadramawt na al-Mahrah, hali ikawa ngumu sana. Rais wa STC Rashad al-Alimi alisitisha makubaliano ya pamoja ya ulinzi na Imarati na kudai kwamba iondoe vikosi vyake kutoka Yemen ndani ya masaa 24. Saudi Arabia ilimuunga mkono mara moja na kushambulia silaha za Imarati katika Bandari ya Mukalla. Kisha Saudi Arabia ilidai kwamba Imarati itii matakwa ya Rashad al-Alimi na kuondoa vikosi vyake kutoka Yemen. Imarati baadaye iliondoka, na hatimaye, al-Zubaidi alikimbilia Imarati. Kwa hivyo, ni nini kilicho nyuma ya kuongezeka huku kwa mgogoro wa Yemen? Je, Uingereza inapoteza washirika wake nchini Yemen? Na je, mzozo huu una vipimo vya kimataifa?

**Jibu:**

Ili kufafanua mambo, tutaelezea jinsi mgogoro huu ulivyoanzishwa, na kisha yale ambayo matokeo na hali za matukio haya zitasababisha:

**Kwanza: Kipimo cha ndani cha uundaji wa mgogoro:**

1- Kwa juu juu, mgogoro ulianza kuchukua sura wakati Baraza la Mpito la Yemen, ambalo ndilo lililounga mkono zaidi mradi wa kuregesha hali ya Yemen Kusini, lilipotuma vikosi vyake kukamata udhibiti wa Hadramawt na Al-Mahrah na kuwafukuza vikosi vya Muungano wa Kikabila unaoongozwa na Amr bin Habrish kutoka kwenye vituo vya mafuta. “Vikosi vya Yemen vilivyo tiifu kwa Baraza la Mpito la Kusini vilitangaza udhibiti wao, alfajiri ya Alhamisi, wa maeneo yanayomilikiwa na makampuni ya mafuta katika eneo la Al-Masila la Jimbo la Hadramawt, kufuatia kupelekwa kwa majeshi ambako kulijumuisha viwanja vya mafuta, vituo vinavyovizunguka, na njia za usambazaji. Hii ilikuja baada ya kuondolewa kwa vikosi vya Muungano wa Kikabila wa Hadramawt kutoka kwenye nafasi zao katika eneo hilo, kufuatia mapigano machache katika baadhi ya maeneo...” (BBC, 4/12/2025).

2- Al Jazeera iliripoti mnamo 3/12/2025, kwamba ujumbe wa Saudia ukiongozwa na Mohammed al-Qahtani ulifika Mukalla, mji mkuu wa jimbo la Hadramawt, na kuwaleta pamoja wahusika huko. Makubaliano yalifikiwa ili kukomesha ongezeko hilo, na mkataba wa makubaliano ukasainiwa. “Afisi ya Habari ya Gavana wa Hadramawt ilisema katika taarifa kwamba makubaliano hayo yalitiwa saini na Gavana wa Hadramawt, Salem Ahmed al-Khanbashi, na Sheikh Amr bin Ali bin Habrish, Naibu Gavana wa Kwanza na Mkuu wa Muungano wa Makabila ya Hadramawt.” (Sky News, 4/12/2025). Ilikubaliwa kwamba ujumbe wa Saudia ungebaki Hadramawt ili kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano hayo.

3- (Sheikh Amr bin Habrish, mkuu wa Muungano wa Kikabila wa Hadhramaut, ambao unadai utawala huru kwa jimbo la mashariki mwa Yemen lenye utajiri wa mafuta, alisema kwamba Hadhramaut inakabiliwa na uvamizi wa kigeni wenye silaha unaolenga maeneo kwenye pwani na bonde la juu na kutishia vituo vyake vya mafuta. Katika hotuba iliyorushwa kwenye televisheni, bin Habrish alituhumu vikosi vya Baraza la Mpito la Kusini kwa “kuanzisha shambulizi la hila dhidi ya nafasi za Muungano wa Kikabila wa Hadhramaut, kwa kutumia droni katika ukiukaji wa wazi wa makubaliano yaliyofikiwa kati ya muungano huo na mamlaka ya ndani katika jimbo la Hadhramaut, ambayo yalisababisha vifo na majeraha.” (Al-Araby Al-Jadeed, 9/12/2025)).

Saudi Arabia ilipinga matukio haya. [Meja Jenerali Mohammed Al-Qahtani (mkuu wa kamati maalum inayohusika na Yemen), na mkuu wa ujumbe wa Saudi Arabia unaotembelea Jimbo la Hadhramawt kwa sasa, alisisitiza msimamo wa nchi yake kuunga mkono utulivu wa jimbo hilo, na akapinga “majaribio yoyote ya kulazimisha kitendo kilichotekelezwa kwa nguvu”].

4- Wakati huo huo, mkuu wa Baraza la Uongozi la Rais wa Yemen, Rashad al-Alimi, alipitisha msimamo unaoendana na Saudi Arabia. “Al-Alimi alithibitisha kukataa kwake kwa kina vitendo vyovyote vya upande mmoja vinavyovuruga usalama na utulivu na kudhoofisha mamlaka ya serikali halali, akisisitiza haja ya kufuata kikamilifu makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyofikiwa katika Jimbo la Hadramawt. Kauli za Al-Alimi zilitolewa kabla ya kuondoka kwake kutoka mji mkuu wa mpito, Aden, hadi Ufalme wa Saudi Arabia.” (Gazeti la Al-Quds, 5/12/2025).

5- Wakati juhudi za Saudi Arabia za kuregesha hali hiyo kama ilivyokuwa kabla ya Imarati kupeleka vikosi vya Baraza la Mpito la Kusini huko Hadramawt na Al-Mahrah kushindwa, na kufikia mwisho mbaya, mgogoro ulizidi na kuchukua vipimo vya kikanda. "Mnamo Jumanne, Rashad Al-Alimi, mkuu wa Baraza la Uongozi la Rais nchini Yemen, alitoa uamuzi wa kufuta makubaliano ya pamoja ya ulinzi na Imarati na kuvipa vikosi vya Imarati masaa 24 kuondoka Yemen." (RT, 30/12/2025). Pia aliamuru Vikosi vya Ngao ya Nchi (vinavyoshirikiana na Wizara ya Ulinzi) kusonga na kuchukua kambi zote zilizo katika majimbo hayo mawili.

6- Saudi Arabia iliunga mkono hatua hii mara moja, na mgogoro ukazidi kuwa mbaya. Vikosi vya Saudi Arabia vilipiga mabomu silaha na zana zilizotumwa na Imarati hadi Bandari ya Mukalla ili kuunga mkono Baraza la Mpito la Kusini. "Muungano unaoongozwa na Saudi Arabia nchini Yemen ulitangaza mnamo Jumanne kwamba ulikuwa umefanya operesheni ndogo ya kijeshi inayolenga silaha na magari ya kivita ambayo yalikuwa yamewasili kutoka Imarati katika Bandari ya Mukalla katika Jimbo la Hadramawt." (Sada News, 30/12/2025). Hivyo, mgogoro mkubwa ulizuka Yemen, ambao juhudi za kidiplomasia zilishindwa kuutatua, na ukazidi kuwa mbaya kikanda. Saudi Arabia ilidai Baraza la Rais liifukuze Imarati kutoka uwanja wa Yemen, na kisha kulipua silaha ambazo Imarati ilikuwa imetuma kwa Baraza la Mpito la Kusini huko Hadramawt, na kutishia mgogoro mkubwa kati ya Saudi Arabia na Imarati sawa na kile kilichotokea kati ya Saudi Arabia na Qatar mnamo 2017.

7- Vitisho hivyo viliendelea hadi Imarati "ilipowasilisha" na kutangaza kujiondoa kwa vikosi vyake kutoka Yemen. "Wizara ya Ulinzi ya Imarati ilitangaza mnamo Jumanne kusitishwa kwa timu zilizobaki za kupambana na ugaidi nchini Yemen kwa hiari yake, kuhakikisha usalama wa wafanyikazi wake, na kwa ushirikiano na washirika husika..." (RT, 30/12/2025). Saudi Arabia iliendelea kutoa maonyo kwa washirika wa Imarati nchini Yemen (Baraza la Mpito la Kusini linaloongozwa na Aidarus al-Zubaidi) kujiondoa kutoka Hadramawt na al-Mahrah. Hapo awali Baraza lilikataa kufuata sheria, lakini kisha likaanza kuonyesha kufuata sheria chini ya shinikizo la Saudia, likitoa uwepo wa pamoja au kujiondoa kivipande. "Vikosi vya Baraza la Mpito la Kusini nchini Yemen vilianza kujiondoa kutoka maeneo kadhaa katika pwani na bonde la Hadramawt..." (Al-Modon, 31/12/2025). Kujiondoa huku hakukuwa suluhisho la mwisho la mgogoro huo, bali udanganyifu!

8- Kisha, Al-Zubaidi alikimbia kutoka Aden hadi Abu Dhabi kupitia Somaliland mnamo 8 Januari 2026, kulingana na tangazo la vyombo vya habari la muungano huo. Waziri wa Ulinzi wa Saudia kisha akasema kwamba "Ufalme, kwa kushauriana na watu wa kusini, utaunda kamati ya maandalizi ya kuandaa kongamano la Riyadh." Mnamo Ijumaa asubuhi, Abdul Rahman Al-Subaihi, Katibu Mkuu wa Baraza la Mpito la Kusini nchini Yemen, alitangaza kuvunjwa kwa baraza hilo na vyombo vyake vyote, akitangaza "kwamba watafanya kazi ili kufikia lengo la haki la kusini kupitia kongamano pana la kusini chini ya ufadhili wa Ufalme wa Saudi Arabia." (Al Jazeera, 9/1/2026).

**<u>Pili: Kipimo cha kimataifa</u>**

1- Kipimo hiki ni wazi na hakina utata. Watawala wa Saudi Arabia ni vibaraka wa Amerika, wanaotekeleza sera zake, na watawala wa Imarati (UAE) ni vibaraka wa Uingereza, wanaotekeleza sera za Uingereza. Wako pande tofauti, kwa hivyo maslahi yao yanagongana nchini Yemen, na wanasimama ukingoni mwa mzozo au wanaingia katika moja ya milango yake. Hata hivyo, pande za Yemen zinazohusika katika mzozo huu, hadi hivi karibuni, zote zilikuwa vibaraka wa Uingereza. Aidarus al-Zubaidi, anayeongoza Baraza la Mpito kusini mwa Yemen na ni mmoja wa wanachama wanane wa Baraza la Rais, ni kibaraka wa Uingereza na anaratibu vitendo vyake vyote na Imarati (UAE).

2- Kuhusu Rashad al-Alimi, rais wa Baraza la Uongozi wa Rais, yeye pia aliwahi kuwa na uhusiano na Waingereza, lakini aliunga mkono Saudi Arabia kwa nguvu na kuitaka Imarati iondoke Yemen. Imarati ni chombo chenye nguvu cha Uingereza cha kudumisha ushawishi wake nchini Yemen.

**Kufafanua:**

a- Mnamo 2022, Baraza la Uongozi wa Rais lilianzishwa, huku Rashad al-Alimi akishikilia mamlaka ya urais, huku wanachama wengine saba wakishikilia mamlaka ya makamu wa rais. Saudi Arabia na mwakilishi wa Marekani alikubaliana na kuundwa kwa baraza hili la rais, licha ya wanachama wake wengi kutoka taasisi ya kisiasa ya Yemen inayoegemea kwa Waingereza. Hata hivyo, hawakuwa na wasiwasi kwa sababu Saudi Arabia ilidhibiti baraza hilo kupitia usaidizi wa kifedha na usalama, hasa kwa vile lilijumuisha wanachama wanne kutoka Baraza la Mpito la Kusini ili kulituliza. Zaidi ya hayo, al-Alimi, ambaye alikuwa mshirika wa Uingereza na alikuwa na nyadhifa za kisiasa za juu tangu enzi ya Rais wa zamani wa Yemen Ali Abdullah Saleh, aliishi nchini Saudi Arabia na alitegemea sana misaada ya kifedha na usalama ya Saudi Arabia. Yote haya yaliipa Saudi Arabia nguvu kubwa juu yake, ambayo imeongezeka sana katika siku za hivi karibuni.

b- Kwa hivyo, msimamo wake ulikuwa mkali katika kupinga shambulizi lililoanzishwa na Baraza la Mpito la Kusini kwenye majimbo ya Hadramawt na Al-Mahrah mwanzoni mwa Disemba. Hakuishia hapo, lakini pia alichukua msimamo mkali akitaka Imarati iondoke kwenye uwanja wa Yemen. Hii inasababisha uharibifu mkubwa kwa ushawishi uliobaki wa Uingereza nchini Yemen. Hii inaonyesha mabadiliko ya utiifu, na taarifa yake ya hivi karibuni inaonyesha zaidi, ikiwa si kuthibitisha, hili: "Mkuu wa Baraza la Uongozi wa Rais nchini Yemen, Rashad al-Alimi, alisema leo kwamba kulinda ushirikiano wa kimkakati na Saudi Arabia ni jukumu la kitaifa. Uongozi wa Yemen unaelewa mafanikio unayopata na pia unafahamu hatari za kuuhatarisha, ukisisitiza kwamba ushirikiano huu ni nguzo ya msingi katika kuunga mkono juhudi za kuregesha dola ya Yemen." (Al-Arabiya, 1/1/2026). Kutokana na hayo, vibaraka wakuu wa Uingereza ndani ya Baraza la Rais walimshambulia, wakidai alikuwa akitenda zaidi ya mamlaka yake. Walitoa taarifa ya pamoja wakisema kwamba ("walifuatilia kwa wasiwasi mkubwa hatua na maamuzi ya upande mmoja yaliyochukuliwa na mkuu wa Baraza la Uongozi wa Rais, Rashad al-Alimi, ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwa hali ya hatari na kutolewa kwa matamko ya kisiasa na usalama. "Hatari, hata kufikia hatua ya kudai kwamba Imarati inapaswa kufukuzwa kutoka muungano wa Kiarabu na kutoka eneo la Yemen." (Independent Arabia, 30/12/2025)). Hata hivyo, mabadiliko ya utiifu wa Al-Alimi kutoka Uingereza hadi Saudi Arabia hayamaanishi mwisho wa ushawishi wa Uingereza huko Yemen Kusini, lakini yameidhoofisha, hasa baada ya Abdul Rahman Al-Subaihi kutangaza kuvunjwa kwa Baraza la Mpito la Kusini.

**Tatu: Baada ya kuchunguza mzozo huu mkali, tunaona kwamba unazunguka pambizoni mwa Hadramawt na, kisha, Jimbo la Al-Mahrah:**

1- Hadramawt, ambayo inajumuisha takriban theluthi moja ya Yemen, ilibaki pambizoni mwa mzozo katika miaka yote ya vita vya Yemen. Ilizingatiwa waziwazi kuwa ndani ya maeneo yanayodhibitiwa na Baraza la Mpito la Kusini, ambalo linatafuta kutenganisha kusini mwa Yemen na kaskazini. Uingiliaji kati wa Saudia huko ulikuwa mdogo. Mnamo 2024, Saudi Arabia iliunga mkono kuingia kwa vikosi vya serikali ya Yemen (Rashad al-Alimi) katika Hadramawt, huku Baraza la Mpito la Kusini linaloungwa mkono na Imarati likipinga hili. (tovuti ya Balqees, 3/6/2024). Uingiliaji kati wa Saudia huko Hadramawt ulibaki mdogo hadi Trump alipoingia madarakani nchini Amerika, ambapo uingiliaji kati wa Saudia uliongezeka na kufikia kilele chake katika vitisho vya hivi karibuni dhidi ya Imarati na Baraza la Mpito la Kusini.

2- Kuhusu uingiliaji kati ulioongezeka wa Saudia huko Hadramawt baada ya utawala wa Trump kuchukua madaraka, ni dhahiri kabisa. Tangu mwanzoni mwa 2025, Saudi Arabia imekuwa na ushawishi mkubwa huko Hadramawt, ikiwasiliana na viongozi wa kikabila na kukuza wafuasi. Ilipata mshirika wake bora, Amr bin Habrish, kiongozi wa Muungano wa Kikabila wa Hadramawt na Naibu Gavana wa Kwanza wa Hadramawt. Saudi Arabia ilimpa msaada na kumpa nguvu, na kumfanya atafute udhibiti na utawala mkubwa huko Hadramawt. (Mnamo Februari 2025, bin Habrish aliendeleza shughuli zake kwa kuunda "Vikosi vya Ulinzi vya Hadramawt," sanjari na tangazo la kusimamishwa kwa usafirishaji wa mafuta. (Al Jazeera Net, 3/12/2025)). Kisha alipokelewa na maafisa wakuu jijini Riyadh, wakiwemo Waziri wa Ulinzi na Mkuu wa Jeshi la Saudi Arabia, baada ya Saudi Arabia kutuma ndege ya kijeshi kumsafirisha kutoka Seiyun hadi Riyadh na kumpatia msaada mwingi (Gazeti la Al-Arab, 29/3/2025). Aliporudi kutoka Riyadh, alitangaza mnamo Mei 2025 kuanzishwa kwa vikosi sita vya kijeshi vyenye wapiganaji 35,000, na kuundwa kwa vitengo vipya, vikosi maalum vya usalama, kama vile huduma za usalama na uokoaji binafsi, na hatimaye, Saudi Arabia ilimsukuma mtu wake, Amr bin Habrish, kuchukua udhibiti wa makampuni ya mafuta, ambayo ndiyo yaliyokuwa kikwazo kilichovunja mgongo wa ngamia kwa Baraza la Mpito lililoongozwa na Aidarus al-Zubaidi, kwa hivyo alikunja mikono yake ili kumrudisha Hadramawt chini ya udhibiti wake, jambo lililochochea mgogoro huo.

3- Kisha kuna jambo jengine, ambalo ni kwamba Jimbo kubwa la Hadramawt liko juu ya hazina ya thamani ya utajiri wa madini asilia, ikiwa ni pamoja na madini adimu ya ardhini kama vile scandium, ambayo iligunduliwa kwa wingi katika wilaya za pwani za Hadramawt za Brom Mayfa na Hajar. Scandium hutumika katika utengenezaji wa ndege na vyombo vya anga, kama ilivyothibitishwa na tovuti ya Jiji la Aden, 7/11/2025, ikinukuu Mamlaka ya Utafiti wa Jiolojia jimboni Hadramawt. Ugunduzi huu huko Hadramawt ungeiweka Yemen kwenye ramani ya kimataifa ya madini adimu ya ardhi. Zaidi ya hayo, mchanga mweusi wa Hadramawt una madini mengi kama vile ilmenite, rutile, zircon, na magnetite, ambayo makampuni ya kimataifa yanashindana kuwekeza. Pia kuna mafuta, marumaru, na granite huko Hadramawt. "Hata hivyo, Yemen inajitokeza kama nchi pekee ya Kiarabu ambayo imejipatia nafasi kwenye orodha ya nchi zinazozalisha madini adimu ya ardhi katika Mashariki ya Kati..." (Jukwaa la Nishati, lenye makao yake makuu jijini Washington, 8/7/2025). Madini haya adimu ya ardhi ndiyo yameisukuma utawala wa Trump katika sera zake nyingi za kimataifa ili kukabiliana na utawala wa China juu ya madini haya adimu ya ardhi, ambayo yanatawala michakato nyeti wa viwanda kama vile chipsi za kielektroniki.

4- Kwa hivyo, inakuwa wazi kwamba utawala wa Trump ndio ulioisukuma Saudi Arabia kuharibu utulivu wa Hadramawt. Majaribio ya muungano wa kikabila, ukiongozwa na Bin Habrish, ya kunyakua udhibiti wa makampuni ya mafuta na kuongeza miito ya uhuru wa kujitawala yalisababisha kundi linaloungwa mkono na Uingereza (Imarati na washirika wake wa ndani, kama vile Baraza la Mpito la Kusini) kushambulia na kuteka Hadramawt, pamoja na Jimbo la Al-Mahrah. Hii iliisukuma Saudi Arabia, au tuseme utawala wa Trump, katika hali ya wasiwasi, na kusababisha hatua kali dhidi ya Imarati—hatua ambazo hazijawahi kutokea tangu muungano wao katika Operesheni ya Kimbunga cha Maamuzi mnamo 2015. Hatua hizi kali zilijumuisha kulipua silaha za Imarati na kutishia washirika wake katika Baraza la Mpito la Kusini. Hii inaonyesha uzito mkubwa ambao utawala wa Trump unaliona suala hili—suala la madini adimu huko Hadramawt. Amerika haiko nje ya picha, hata kama ina imani na chombo chake cha Saudia. Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Marco Rubio aliwasiliana na Waziri wa Mambo ya Nje wa Saudia Faisal bin Farhan "wakati ambao walijadili hali nchini Yemen na masuala yanayoathiri usalama na utulivu wa kikanda." (RT, 30/12/2025).

**Nne: Kwa kumalizia, maendeleo mapya katika eneo la Yemen ni kwamba utawala wa Trump unalenga Hadramawt kwa sababu ya madini yake adimu ya ardhi,** ambayo yangeiwezesha Amerika kupambana na udhibiti wa China katika sekta hii nyeti ambayo inasimamia operesheni za viwanda. Hili pia huenda likasababisha mabadiliko katika utiifu wa viongozi wa Yemen kutoka Uingereza hadi Amerika, hasa Rais Rashad al-Alimi. Ikumbukwe kwamba makampuni ya China tayari yanachunguza madini adimu huko Hadramawt, kwa hivyo kupata madini haya ni jambo la dharura kwa Trump kabla ya China kupata udhibiti juu yake. Hivyo, vibaraka wa mataifa makafiri wanachochea mapigano nchini Yemen ili kufikia malengo ya mabwana zao. Msururu huu wa matukio ya kusikitisha unaendelea si tu nchini Yemen bali pia nchini Sudan na nchi zengine za Kiislamu, ambapo Waislamu wanauana katika mizozo ambayo watawala wao vibaraka wanawashawishi kuwa ni kwa maslahi yao, wakiwahimiza kutoa muhanga kila kitu. Hata hivyo, mizozo hii kwa kweli inapiganwa kwa ajili ya kutetea maslahi ya mataifa ya makafiri. Msururu huu utaendelea hadi kundi lenye nguvu zaidi katika Umma litakapoinuka, liwashinde watawala wake, liwahisabu vikali, na kuasisi hali ya uadilifu, huruma, na mwongozo—Dola ya Khilafah itaanzishwa kwa mujibu wa utaratibu wa Utume, baada ya hapo kutakuwa na kila chema ambacho Mwenyezi Mungu atakipenda kwa Uislamu na Waislamu, baraka kutoka mbinguni, neema, utukufu, na heshima.

﴿إِنَّ اللَّهَ بَالِغُ أَمْرِهِ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْراً﴾

**"Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake."** [At-Talaq: 3]

Na kesho iko karibu kwa wale wenye kusubiri.

**22 Rajab 1447 H**

**11 Januari 2026 M**